# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA TANO

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 31 Oktoba, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubahi)*

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

### TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nafurahi sana kuwakaribisha hapa Dodoma katika Mkutano wetu wa Tano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninayo taarifa, Bunge katika Mkutano wake wa Nne pamoja na shughuli za kupitisha Bajeti za Serikali na Makadirio ya Matumizi na Mapato ya Wizara mbalimbali ilipitisha pia Miswaada ya Sheria ya Serikali ifuatayo:-

(i) *The Finance Bill* ya mwaka 2006; na
(ii) *The Appropriations Bill* ya mwaka 2006.

Nafurahi kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge, kwamba Miswada hiyo tayari imepata kibali cha Mheshimiwa Rais mnamo tarehe 30 Septemba, 2006 na sasa *Finance Bill* ni Sheria namba sita ya mwaka 2006 na *The Appropriations Bill* ni Sheria namba saba ya mwaka 2006. Ahsante. *(Makofi)*

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

### MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

**Utekelezaji wa Sheria ya *The Dodoma Special Investment Area, Act 1989***

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1989 Serikali ilitunga Sheria iitwayo *The Dodoma Special Investment Area Act 1989* iliyokuwa na lengo la kuhamasisha ujenzi wa Makao Makuu kwa kuvutia wawekezaji, ujenzi wa makazi na uboreshaji miundombinu; na kwa kuwa Serikali imetamka kuwa itaongeza kasi ya kujenga mazingira muafaka katika kuharakisha uhamiaji wa Dodoma:-

(a) Je, kasoro gani zilizoathiri utekelezaji wa Sheria hiyo?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani katika kuirekebisha Sheria hiyo ili iweze kukidhi madhumuni yaliyokusudiwa?

(c) Je, Serikali inafanya maandalizi gani ya kuendeleza matumizi ya Sheria hiyo baada ya muda wake kumaliza ifikapo mwaka 2009 hasa ikizingatiwa kuwa msukumo wake bado unaendelea kuhitajika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Sheria ya Bunge ya kuhamasisha ujenzi wa Makao Makuu kwa lengo la kuvutia wawekezaji, ujenzi wa makazi na uboreshaji wa miundombinu ilitungwa mwaka 1989. Hata hivyo kumekuwepo na kasoro kadhaa zilizoathiri utekelezaji wa sheria hii. Kasoro hizo zinajitokeza katika maeneo yafuatayo:-

(i) Vifungu Na. 13 na Na. 15 kuhusu unafuu wa asilimia 50 katika gharama za maji na umeme.

(ii) Kifungu Na. 16(i) kuhusu nafuu ya kodi katika biashara zilizoainishwa ambayo inatoa tafsiri zenye maana nyingi.

(iii) Kampuni Tanzu za Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu ambazo zililengwa kupata msamaha wa kodi ya mapato na kutoa mchango mkubwa katika uendelezaji Makao Makuu kwa sasa hazipo, zimefilisiwa kutokana na Sera ya Serikali ya kujitoa katika biashara. Aidha, hapakuwa na chombo mbadala kutekeleza majukumu ya kampuni hizo.

(iv) Sheria haitoi tafsiri ya mwekezaji *(Investor)* hali kadhalika tafsiri ya mradi maalum *(Special Investments).*

(b) Mheshimiwa Spika, jitihada za Serikali kufanya marekebisho katika Sheria hii imekuwa ni kupitia upya Sheria ya Uwekezaji kwa kuboresha kuondoa kasoro kadhaa na kuipa sura mpya inayoendana na mazingira ya sasa.

(c) Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisho hayo yanakusudia kupitisha Sheria mpya itakayochukua nafasi ya ile ya mwaka 1989.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Waziri alikiri kwamba kuna mapungufu mengi sana katika ile Sheria, je, Serikali iko tayari kutamka bayana ni lini hiyo sheria itarekebishwa?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunatatizo la sauti, Wahandisi wanaendelea kurekebisha lakini halizuii kazi yetu kuendelea.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Spika, kwa kawaida kuna utaratibu wa kupitisha sheria, tunaamini Serikali haiwezi kutamka mara moja kwamba ni lini hiyo Sheria itapitishwa, lazima ipitie mchakato wa taratibu za utunzi wa Sheria katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruksa yako swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sio Sheria peke yake inaweza kusaidia wawekezaji kwenda kuwekeza tatizo kubwa ni miundombinu ndiyo inaweza kumvutia mwekezaji kwenda kuwekeza. Je, haoni wakati umefika sasa kwa kuwa kuna kampeni kubwa hivi sasa kila Mikoa kutangaza maeneo yao ya kuwekeza kwamba Serikali sasa ijikite katika kuendeleza miundombinu ili kuwafanya wawekezaji waweze kwenda kuwekeza badala ya kupitisha Sheria ambazo kimsingi haziwezi kutekelezeka?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo la msingi katika kuleta ufanisi wa maendeleo na hali ni miundombinu. Hivi sasa Serikali imefanya jitihada kubwa ya kuweza kuunganisha Mji na Mkoa wa Dodoma kwa barabara. Hivi sasa inajengwa barabara nzuri kutoka hapa kwenda Singida na wote ni mashahidi na vile vile kuna mipango thabiti ya kuweza kuunganisha barabara ya kutoka Arusha - Babati kuendelea mpaka Iringa. Serikali inaimani kwamba miundombinu hii ikikamilika hapa Dodoma patakuwa na maendeleo makubwa kwa sababu ya barabara ambazo zimeanza kujengwa. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri lakini nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Sheria hii ya *The Dodoma Special Investment Act* ya mwaka 1989, maudhui yake yanafanana sana na ile *Special Economic Zone Act* ya mwaka 2006, je, Serikali haioni kwamba kwa sababu hizi hizi kuna haja ya Dodoma kuwa *Special Economic Zone? (Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli alilolisema Mheshimiwa George Simbachawene na Serikali imeitaka Mikoa mingine yote pamoja na Dodoma kuweza kuitisha vikao vya uwekezaji na wafanyabiashara mbalimbali ili waweze kubuni utaratibu mzuri wa kuweza kufanya maeneo yao yaweze kufanikiwa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, lakini alilolisema ni kweli, jitihada za Serikali zinaendelea kwa Mikoa mbalimbali kufanya maeneo maalum ya uwekezaji na wakati ukifika pia na maeneo ya Dodoma na Mikoa mingine inaweza kuwa mojawapo lakini tunafanya hatua hizi. Nashukuru sana kwa kutukumbusha hilo lakini Serikali imeliona na itaendelea kama inavyoendelea kufanya matayarisho ya maeneo mengine. *(Makofi)*

Na. 2

**Tatizo la Gari la Wagonjwa Hospitali ya Wilaya ya Kisarawe**

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO** aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi nimekuwa nikieleza Serikali tatizo la ukosefu wa magari ya kubeba wagonjwa katika hospitali ya Wilaya ya Kisarawe na kwenye vituo vya Afya vya Maneromango na Mzenga; na kwa kuwa swali la mwisho juu ya tatizo hili lilikuwa la nyongeza kwa swali Na. 12 lililoulizwa tarehe 9 Juni, 2004; na kwa kuwa Waziri aliahidi kulishughulikia tatizo hili mara Serikali ipatapo uwezo:-

Kwa kuzingatia kuwa sasa Serikali inakusanya kodi ya shilingi bilioni 195 kwa mwezi badala ya shilingi bilioni 100 za wakati ule; je, Serikali haioni kuwa sasa wakati umefika wa kulitatua tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukubaliana na Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe kuwa kiwango cha makusanyo ya kodi nchini kimeongezeka. Aidha, nakubaliana nae pia kwamba Serikali iliahidi kutoa gari la kubeba wagonjwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe mwaka 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Serikali ilinunua magari 22 ya kubeba wagonjwa. Magari hayo yaligawiwa kwa Halmashauri mpya na zilizopo pembezoni. Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe haikupata gari katika mgao huo. Hata hivyo, hospitali ya Kisarawe inalo gari la kubeba wagonjwa lenye namba STH 9265 ingawa haliko katika hali nzuri. Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Ofisi yangu imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.2 kununua magari ya kubeba wagonjwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe imo katika orodha ya Wilaya zitakazopatiwa gari

moja. Gari hilo litakapopatikana, Halmashauri itaangalia ni wapi watapeleka ambako kuna tatizo kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza tatizo la magari ya kubeba wagonjwa, natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kutenga fedha katika Bajeti zao kwa ajili ya kununua na kukarabati magari ya aina hiyo. Aidha, Halmashauri ziwalisiliane na wahisani na marafiki mbalimbali ambao wako tayari kusaidia kutoa magari ya kubeba wagonjwa.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ambayo sikuridhika nayo, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali moja au mawili ya nyongeza.

(a) Je, anajua kwamba Kisarawe kiuchumi iko pembezoni?

(b) Pamoja na kwamba hospitali ya Kisarawe iko karibu umbali wa kilometa 30 kutoka hospitali ya Muhimbili inapokea wagonjwa wengi kutoka Kisarawe na kutoka Wilaya ya Ilala, je, atakubaliana na mimi kwamba umuhimu wa kupatikana gari licha ya kutoka katika Zahanati kupelekwa hospitali ya Wilaya kuna haja ya kuwachukua wanaougua kutoka pale kwenda katika Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe itapatiwa gari moja kwa mwaka wa fedha huu.

Kwa hiyo, ahadi Mheshimiwa Mbunge naomba aichukulie kwamba ni ya ukweli na gari watapatiwa ili kuhakikisha kwamba tatizo kama halitapungua kabisa, lakini angalau litasaidia kwa njia moja au nyingine katika Wilaya hiyo. Tunafahamu kwamba Kisarawe inahitaji gari la aina hiyo ndio maana tumewapata kipaombele kwa mwaka huu kwamba tutawapatia gari hilo. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri yenye matumaini ya Mheshimiwa Naibu Waziri, je, kwa kuwa tuna Wilaya mpya ambazo hazina magari na zipo katika maeneo magumu, je, Serikali itawapa kipaumbele Wilaya hizo mpya ambazo hawana magari ya hospitali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwa jibu langu la msigni kwamba magari 30 ambayo yamenunuliwa mwaka huu, kipaumbele ni kwa zile Wilaya mpya na Wilaya zile ambazo ziko pembezoni. Kwa hiyo, zile Wilaya mpya na Wilaya ambazo ziko pembezoni na zinafahamika watapatiwa magari hayo ambayo kwa sasa ni *process* ya kukombolewa kule bandarini.

Na. 3

**Utunzaji wa Nyaraka**

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI** aliuliza:-

Kwa kuwa suala la kuhifadhi nyaraka ni muhimu duniani kote; na kwa nchi kuwa na kumbukumbu zake ni muhimu zaidi.

(a) Je, Serikali imefanya juhudi gani za ziada za kuongeza idadi ya nyaraka za watu binafsi zenye umuhimu wa historia ya nchi yetu ili kuhifadhiwa vizuri; kama zile za Hayati Baba wa Taifa Mwalimu J. K. Nyerere, Marehemu H. T. Seleman, Marehemu Mzee Rajabu Diwani na Alhaji Mzee Mustafa Songambele?

(b) Kama ziko nyaraka zilizoongezeka, je, zile za Mzee wetu Rashid Mfaume Kawawa zipo?

(c) Je, kuna mpango wowote wa kuwapa tuzo wazee hao ili kuwapa hamasa wazee wengine wafanye hivyo na hasa Marehemu H. T. Seleman ambaye aliweza kuhifadhi nyaraka pekee za *African Association?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria ya kuwaenzi Waasisi wa Taifa *(The Founders of The Nation Honouring Procedures Act)* Na. 18 ya 20004 pamoja na Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Na. 3 ya mwaka 2002 Serikali inao utaratibu wa kisheria wa kuhifadhi baadhi ya nyaraka za watu mbalimbali kama vile Baba wa Taifa na mengine zenye umuhimu kwa Taifa letu kihistoria, kisiasa, kiuchumi na kijamii.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishafanya mahojiano na Mzee Rashid Mfaume Kawawa na mazungumzo hayo tayari yamekwisha hifadhiwa. Hali kadhalika Serikali inafanya taratibu za kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zake ambazo ziko katika maandishi kwa umuhimu wa pekee kutokana na mchango wake kwa Taifa na kwa ajili ya matumizi ya sasa na ya baadaye.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haijaanza kuwa na utaratibu wa kutoa tuzo kwa wazee kama vile Mzee Hassani T. Suleiman aliyehifadhi nyaraka mbalimbali za *African Association*.

Mheshimiwa Spika, napenda kupitia Bunge lako Tukufu kuwaomba wananchi wenye nyaraka muhimu kuwasiliana na Idara ya Nyaraka za Taifa ili kumbukumbu hizo zihifadhiwe.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, mimi swali langu ni dogo tu, nina kama ombi kwa vile hawajaanza hizo harakati za kuweka tunzo, kwa nini kuanzia sasa hivi isiweke hiyo haraka ya kuanza kutoa tunzo kwa watunza nyaraka kwa watunza nyaraka?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunao utaratibu ambao waliotunza kumbukumbu au nyaraka tunaweza kuzipokea kama kwa kuwekeza, lakini pia tunaweza kuzinunua pale ambapo ofisi yangu itakuwa imekubaliana kupitia Wizara ya Fedha, lakini utaratibu wa kutoa tunzo mpaka sasa hivi bado haujafikiwa lakini bado tutaangalia uwezekano huo.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jawabu lake katika suala mama na nina moja la nyongeza, lakini ningemwomba Mheshimiwa Waziri akalifahamisha Bunge letu Tukufu kwa sababu tuko katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivi kuna utaratibu gani kwa Wizara yake kutunza kumbukumbu kama vile za Mheshimiwa Sheikh Thabiti Kombo na Mzee Abeid Karume na hivi sasa kumbukumbu hizo au nyaraka hizo zinatunzwa wapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, sasa hivi ofisi yangu iko katika mchakato wa kutafuta eneo la kuanzisha kituo cha kuwaenzi waasisi ambapo Sheikh Abeid Karume pamoja na waasisi wengine.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kufahamu kuna utaratibu gani kwa watu ambao wamelitumikia Taifa hili katika sehemu nyeti na wana kumbukumbu nyingi ambazo hazikuandikwa katika sehemu nyeti, na wana kumbukumbu nyingi ambazo hazikuandikwa, lakini wangetaka kuziandika, wanatakiwa wafanye nini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwa wale waasisi na watu wengi ambao wana kumbukumbu muhimu ambazo wangependa zihifadhiwe tungewaomba wawasiliane na ofisi yangu ili tuone kwa kiasi gani tunaweza kuwasaidia ili waweze kuwekesha kumbukumbu hizo.

Na. 4

## Utaratibu wa Uhamisho kwa Wafanyakazi Wanandoa

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI (k.n.y MHE. SHALLY J. RAYMOND)** aliuliza:-

Kwa kuwa tangu Uhuru hadi miaka ya 1970 Serikali ilikuwa na utaratibu mzuri kwa kuruhusu wanandoa na familia zao kuhama kwa pamoja inapotokea uhamisho; na kwa kuwa kuanzia miaka ya 1970 fursa hiyo ya uhamisho ilififia na kwenye miaka ya 1990 fursa hiyo ilikoma na ililazimika mmoja wa wanandoa hao kuomba uhamisho wa aina hiyo ni sawa na kuwatenganisha wanandoa:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kurudisha utaratibu wa zamani wa kuhamisha wanandoa kwa pamoja?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kutohamisha wanandoa pamoja kunachangia, kunadhoofisha maadili na malezi ya watoto ambayo hufanywa kwa pamoja?

(c) Je, Serikali haioni kwa kuwatenganisha wanandoa kunaweza kushawishi maadili ambayo ni potofu na hatimaye kusambaratisha familia, kwa magonjwa na hasa gonjwa la UKIMWI?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kimsingi Serikali haikatazi wanandoa kuhama kwa pamoja. Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 pamoja na marekebisho yake (Sheria Na. 25 ya 2002), sababu zinazosababisha wanandoa kutohamishwa kwa pamoja ni ukosefu wa nafasi katika kituo anachohamishiwa mmoja wao, uhaba wa watumishi katika kituo cha mwanandoa anayelazimika kuhama kumfuata mwenzi wake na uwezekano wa wanandoa hao kuwa katika mamlaka tofauti za ajira.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haifikirii kwamba muda mfupi ambao mmoja wao atakuwa anafuatilia kukamilika kwa taratibu zilizotajwa, kudhoofisha maadili na malezi ya watoto. Endapo familia husika itakuwa imeweka misingi bora ya malezi ya watoto toka mwanzo, maadili ya familia husika katika kipindi cha mpito hayatadhoofika, kwani baada ya muda mfupi familia hiyo itakuwa pamoja. Uzoefu unaonyesha kwamba ni kawaida kwa wanandoa kutokuwa pamoja kwa nyakati mbalimbali mfano mmoja anapokuwa masomoni au safari za kikazi.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haioni kwamba katika kipindi hicho kifupi cha kusubiri kwa wanandoa hao kukamilisha taratibu za kuungana pamoja kunaweza

kusababisha wanandoa washawishike kushiriki katika maadili potofu na hatimaye kuambukizwa magonjwa hatari kama UKIMWI. Suala la msingi kwa wanandoa ni kuwa waaminifu katika ndoa zao na kufuata maadili.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona, kwa kuwa kuna wafanyakazi wengi ambao wamechukua muda mrefu taratibu za uhamisho kufanyika. Je, Serikali haioni kwamba anakataa tama yule mtumishi na kufanya utendaji wake usiwe bora?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba Serikali haikusudii kuwakataza wanandoa kuhama kwa wakati mmoja. Lakini tunachoangalia je, huko ambako mwanandoa mmoja amehamishiwa, huyu mwingine kuna nafasi ya kumhamishia, kwa sababu wakati mwingine unaweza ukakuta kama nilivyosema wako katika mamlaka tofauti ya ajira, labda mwanamke anafanyia kazi katika benki labda ya *Micro Finance* na mwanaume labda ni mtumishi katika Serikali za Mitaa na unakuta sehemu ambayo mwanaume anahamishiwa hakuna benki, kwa hiyo huwezi kusema unawahamisha wote kwa pamoja, hasa ukizingatia mamlaka za ajira ni tofauti, kwa hiyo, jukumu la wanandoa wenyewe kufuatilia uhamisho huo kwa wakati.

Na. 5

**Wanawake Kujifungua kwa Njia ya Upasuaji**

**MHE. LUCY T. MAYENGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imedhamiria kuhakikisha huduma za afya zinatolewa na hospitali zilizopo zinazingatia viwango vya hali ya juu vilivyowekwa:-

(a) Je, ni sababu zipi zinazopelekea baadhi ya hospitali za binafsi kulazimisha uzalishaji wa akinamama wajawazito kwa njia ya upasuaji?

(b) Je, ni hospitali ipi katika Jiji la Dar es Salaam ambayo ina kiwango kikubwa cha akinamama wanaojifungua kwa njia hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kitaalamu upasuaji unafanywa pale tu mzazi anaposhindwa kujifungua kwa njia ya kawaida na upasuaji huo unafanyika ili kunusuru maisha ya mtoto au mama au wote wawili. *(Makofi)*

Tafiti zinaonyesha kwamba katika kituo chenye wataalam na vifaa vya kutosha, upasuaji unafanyika kwa asilimia 5 hadi 15 ya vizazi hai.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa takwimu tulizonazo nchini ni asilimia tatu tu ya vizazi hai inayotokana na huduma ya upasuaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii haina taarifa kuwa hospitali za binafsi zinalazimisha akinamama wajawazito kujifungua kwa njia ya upasuaji, kwani uamuzi wa kutumia njia ya upasuaji hufanywa na mtaalam kulingana na hali ya mgonjwa husika. Iwapo Mheshimiwa Mbunge anazo taarifa za hospitali zinazolazimisha akinamama wajawazito kuzalishwa kwa njia ya upasuaji, nitamwomba tuwasiliane ili Wizara iweze kuzifanyia kazi.

(b) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii haina takwimu zinazohusu kuwapo hospitali binafsi yenye kiwango kikubwa cha akinamama wanaojifungua kwa kulazimishwa kutumia njia ya upasuaji katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, endapo Mheshimiwa Mbunge atahitaji kujua ni hospitali ipi ina kiwango kikubwa cha akinamama wanaojifungua kwa njia ya upasuaji kulingana na ushauri wa kitaalam Jijini Dar es Salaam kwa ujumla, naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam lina idadi ya hospitali 23, zikiwemo hospitali tatu za Manispaa, Hospitali ya Taifa na hospitali 19 za watu binafsi zinazotoa huduma za akinamama wanaojifungua. Kati ya hizi, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ndiyo inayoongoza kwa idadi kubwa ya wanawake wanaojifungua kwa njia ya upasuaji kwa kuwa inapokea rufaa zote kutoka hospitali za Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kumwuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa *justification* ya kujifungua kwa upasuaji ni ngumu kuweza kuthibitika kutokana na kwamba inaweza ikachukuliwa kwamba ni suala la kitalaam lakini vile vile likawa na sababu binafsi. Je, Serikali iko tayari sasa kuweza kufanya utafiti wa kitaalam ili kuweza kubaini hospitali ambazo zimekuwa zikichukulia tatizo hili kama ni suala ambalo ni tatizo la kitaalam lakini vile vile ni suala la kibiashara?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli inawezekana kukawa na dhana kwamba Daktari anaweza akafanya oparesheni kwa njia ambayo anaona yeye ni kwa sababu ya kupata kipato hasa katika hospitali za binafsi.

Lakini nataka kusema tu, kama kweli Daktari anayefanya oparesheni hii anafuata maadili, ni kwamba hawezi kufanya oparesheni, kwa sababu anajua kabisa, kufanya

oparesheni kuna matatizoa mbayo  yanaweza kujitokeza kama atafanya ile oparesheni bila kuwa na *indication*.

Mheshimiwa Spika, lakini siwezi kumkatalia Mheshimiwa Mbunge, isipokuwa ninachotaka kusema ni kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Watalaam tutaweza kulifuatilia suala hili na pale itakapobainika kwamba kuna madaktari au taasisi zozote zinazofanya oparesheni kwa misingi ya kibiashara zaidi, tutaichukulia hatua. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa uzazi wa mpango unasaidia sana kujifungua kwa salama; na kwa kuwa wanaume wengi bado hawajaukubali uzazi wa mpango; je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni sasa ni wakati muafaka kuwashirikisha wanaume wakati wake zao wanapojifungua na wao kuingia *labour room? (Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba uzazi wa mpango ni moja ya njia ambazo zinapunguza kujifungua kwa matatizo.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda tu kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tunaendelea na tunasisitiza sana kuhusu suala la uzazi wa mpango. Lakini vile vile napenda kumfahamisha Mheshimiwa Haroub Said Masoud, kwamba katika shughuli zote nzima tunazoshughulikia kuhusu uzazi wa mpango, Serikali inaendelea na kama ana taarifa ni kwamba siyo tu akinamama wanaopatiwa dawa za uzazi wa mpango, lakini vile vile tunao mpango wa kuweza kufunga uzazi kwa wanaume na hili suala linaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado tunaendelea na tunaangalia ni yupi ambaye anahitajika kufanya uzazi wa mpango. Kama ikionekana kwamba baba anatakiwa asaidie kutokana na afya ya mama, basi huwa tunamshauri baba aweze kufunga uzazi kwa manufaa ya mke wake. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dhana iliyoko ni kuwa kufanya upasuaji daima ni mbaya; na kwa kuwa utafiti uliofanywa katika nchi za Magharibi na hasa *Continental Europe*, inaonyesha kwamba akinamama wengi wanapenda siku hizi kujifungua kwa njia ya *scissor* kuliko njia ya kawaida kwa sababu kuna usalama zaidi; je, Serikali inatoa kauli gani juu ya jambo hilo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika maeneo ya Ulaya watu wengi, akinamama wanapenda kujifungua kwa *scissor*. Swali lake lilikuwa kwamba, je, tunaweza kulitafakari hili suala?

Mheshimiwa Spika, nadhani sisi tunapenda mambo yaende kama yalivyopangwa na Mungu, na pale inapobidi kuwafanyia *scissor*, ndipo tutakapofanya hivyo. Haliwezi likatokea kwenye Wizara yetu tukahamasisha akinamama kwamba twendeni tukawafanyie upasuaji. Hapo itakapofikia mahali wao watakapotaka hiyo, ndiyo utafikia wakati wa kulifikiria hilo suala. *(Makofi)*

Na. 6

**Mradi wa Kusambaza Umeme Mbeya Vijijini**

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa mradi wa kusambaza umeme Mbeya Vijijini ulioanza mwaka 1998 na kusambaza nguzo za umeme katika Kata zote ulifanyika; na kwa kuwa sababu za kusimama kwa mradi huo hazijulikani na kwamba kuna baadhi ya nguzo zimeanza kuharibika au kuibiwa:-

(a) Je, kwa nini mradi huo ulisimama?

(b) Je, mradi huo utaanza lini tena ili kurudisha imani ya wananchi kwa Serikali yao?

**SPIKA:** Namtambua Mheshimiwa Naibu Waziri mpya wa Wizara hiyo ambaye ndiye anayejibu swali hilo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, Mbunge wa Mbeya Vijijini, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mradi wa usambazaji umeme Mbeya Vijijini ulianza mwaka 1998 na ulijumuisha ujenzi wa njia ya umeme ya *KV 33* kupitia Mbalizi/Izumbwe/Horongo/Santilya/Ilembo na Iwiji yenye urefu wa kilometa 44. Mradi huu ulisimama mwaka 2003 baada ya kazi zifuatazo kufanyika:-

- Ujenzi wa njia ya umeme ya Mbalizi/Izumbwe yenye urefu wa kilometa 5 na ufungaji wa transfoma.

- Usimikaji wa nguzo kutoka Izumbwe hadi Santilya ukiwa ni urefu wa kilometa 34; na

- Usimikaji wa nguzo kutoka Izumbwe hadi Horongo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sababu ya msingi iliyofanya mradi huo kusimama ni upungufu wa fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, usambazaji umeme Mbalizi/Izumbwe/Horongo/Santilya/Ilembo na Iwiji umejumuishwa kwenye Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini *(Energizing Rural Transformation)* na shilingi milioni 114 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza mradi huo katika mwaka wa fedha 2006/2007.

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na nina imani kwamba wananchi katika maeneo hayo wamefarijika na hii ikiwa ni awamu ya kwanza, bila shaka baada ya hapo sehemu nyingine zitaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ni kwamba, kitendo cha kusambaza nguzo nyingi za umeme na zikaachwa ziharibike na nyingine labda kuibiwa. Natumaini hili ni tatizo la uharibifu mkubwa sana kwa mali ya Serikali na mali ya wananchi kwa ujumla. Je, Serikali inaliona tatizo hili; na kama inaliona tatizo hili, itazuia tatizo hilo kujitokeza kwa siku zijazo kwa kufanya nini?

Mheshimiwa Spika, la pili, kutokana na tatizo kubwa la umeme tulilonalo sasa hivi; je Serikali haioni kuwa itakuwa vizuri endapo itavuta umeme huo kutoka Zambia ikiwa ni njia mojawapo ya kukuza uhusiano wa kibiaashara katika nchi za Jumuiya ya *SADC?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ubadhilifu unaojitokeza au kurundikana kwa bidhaa au mali ya *TANESCO* sehemu za Mikoani, hii kwa upande mmoja inaweza kuwa inatokana na mipango mibaya ambayo Serikali imekusudia kuiondoa kwa kuhakikisha kuwa tunakuwa na mipango ya kisayansi ambayo kama kutakuwa na mradi wa *TANESCO* unakwenda kwenye vijiji, utakuwa unamalizwa mradi huu kwa kupangiwa bajeti yake na hatutakubali tena mali za *TANESCO* ziwe zinarundikana na kuharibika mikoani.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa ombi kwa Mameneja wote wa *TANESCO* nchini kwamba hilo linapotokea lazima watoe taarifa na lazima kuokoa mali za *TANESCO*. Waheshimiwa Wabunge kama itatokea, mmeona mali za *TANESCO* au za umeme zimerundikana mahali, tuleteeni taarifa mapema ili hatua za kunusuru hali hiyo zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuunganisha umeme kati ya Tanzania na Zambia, mpango huu upo katika awamu ya pili ambayo inaanza mwaka 2010 ya kuleta Megawati 200 kutoka Zambia. Lakini, ni mpango mgumu na unahitaji kwanza kuweka au kuimarisha Gridi ya Taifa ili iweze kubeba mzigo huu kutoka Zambia, lakini pili, itahitaji transforma kama za Mbeya kuimarishwa ili kubeba mzigo huu.

Tatu, itahitaji uchambuzi yakinifu na majadiliano kati ya Tanzania na Zambia kuhusu bei ya umeme huu. Kwa hiyo, hadi hapo mambo haya yote yatakapokamilika, tunategemea kwamba katika mpango wa pili *(Mid term Plan)* ya kuleta umeme Tanzania, suala la kuleta umeme au *connectivity* kati ya Zambia na Tanzania utafanyika mwaka 2010.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nashukuru sana kwa majibu ya Serikali kupitia Naibu Waziri.

Kwa kuwa mazingira haya ya kukosekana umeme katika Kata za Mbeya Vijijini yanafanana au ni sawa kabisa na mazingira yaliyoko Mbinga; je, Naibu Waziri anaweza kutoa matumaini gani kwa wananchi wa Mbinga ambao Kata zao zote hazina umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Wilaya ya Mbinga inakabiliwa na matatizo makubwa ya umeme, lakini kwa bahati nzuri na kwa habari njema, ni kwamba Serikali na Wizara kwanza, ilikuwa imeomba shilingi milioni 500 za kuanza kushughulikia mradi wa kusambaza umeme Mbinga.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa katika kipindi cha mwaka wa fedha bilioni 10.5 kwa ajili ya usambazaji umeme nchini na tunategemea kwamba katika maombi ya Mbinga ya kuleta umeme, kiasi kikubwa kinachokaribia shilingi milioni 500 zitakuwa zimetengwa kwa ajili ya kusambaza umeme Wilaya ya Mbinga. *(Makofi)*

Na. 7

**Matumizi ya Mbolea za Viwandani**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali hutumia kiasi kikubwa cha fedha kununulia na kusambaza mbolea za viwandani *(fertilizers)*; na kwa kuwa mbolea za aina hiyo zisipotumika kwa uangalifu zinaweza kuleta athari kwenye ardhi, mazingira na hata binadamu:-

(a) Je, ni juhudi zipi za makusudi zinazofanywa na Serikali kuhakikisha kuwa elimu sahihi inawafikia watumiaji wa mbolea hizo ili kudhibiti kujitokeza kwa athari hizo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ni busara sasa kuwekeza katika utumiaji wa mbolea ya samadi na mboji badala ya kuendelea na matumizi makubwa ya mbolea hizo za viwandani tusivyokuwa navyo?

(c) Je, hapa nchini yapo maeneo yaliyoathiriwa na mbolea za aina hiyo; na kama yapo Serikali inachukua hatua gani za makusudi za kwasaidia wananchi wa maeneo yaliyoathirika?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mbunge wa Kwimba, swali lake lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya inatoa mafunzo kwa wataalam wa kilimo, mawakala na wasambazaji wa pembejeo juu ya matumizi sahihi ya mbolea kulingana na mapendekezo ya watafiti wa udongo. Ili kudhibiti kuingizwa kwa mbolea zisizokidhi viwango vyenye ubora na kusababisha uharibifu wa ardhi, mazingira na hata binadamu, Serikali inaandaa sheria ya mbolea itakayosimamia udhibiti wa uingizaji, usambazaji, na matumizi sahihi ya mbolea.

(b) Mheshimiwa Spika, pendekezo la Mheshimiwa Mbunge la kutumia mbolea ya samadi na mboji katika kurutubisha ardhi ni zuri na Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inaendelea kuhamasisha wakulima kutumia aina hizo za mbolea.

Hata hivyo, mbolea ya samadi na mboji zina virutubisho vya mmea kidogo ukilinganisha na mbolea za kemikali. Kwa mfano, kwa zao la mahindi, kiasi cha mbolea ya samadi kinachopendekezwa ni tani 15 - 20 kwa hekta ikilinganishwa na kilo 150 - 200 tu au sawa na mifuko 3 - 4 kwa hekta za mbolea ya *Urea*. Ikumbukwe kwamba hakuna hata nchi moja duniani iliyoendeleza kilimo chake kwa kasi kubwa bila kutumia mbolea za kemikali. Mbolea za kemikali zinatumiwa kwa kufuata ushauri wa kitaalam na huu ndiyo ufumbuzi wa nchi yetu kufikia mapinduzi ya kilimo. Kutokana na hali hiyo, inashauriwa mbolea za aina zote zitumike ili kuongeza mavuno kwa lengo la kujitosheleza kwa chakula na ziada kuuzwa kwa ajili ya kuongeza mapato kwa mkulima.

(c) Kwa sasa hatuna takwimu zilizothibitishwa kisayansi kuwa kuna baadhi ya maeneo hapa nchini yaliyoathiriwa na matumizi ya mbolea ya kemikali. Napenda kumtoa wasi wasi Mheshimiwa Mbunge wa Kwimba kuwa matumizi ya mbolea ya kemikali hapa nchini bado yako chini kwa wastani wa kilo nane za virutubisho kwa hekta kwa mwaka ikilinganishwa na mapendekezo ya kitaalam ya kwamba angalau tufikie kilo 60 kwa hekta.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba wale wanaotumia mbolea za chumvi chumvi wanapata mbolea hiyo kwa ruzuku. Je, Serikali ina mpango wowote kama huo kwa wale wanaotumia mbolea ya samadi na mboji ili kuwahamasisha waweze kutumia kwa wingi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika maelezo yangu, mbolea zote aina mbili tunapenda zitumike sambasamba. Kwa hiyo, utaratibu wa kutumia mbolea za kemikali na utaratibu wa kutumia mbolea za mboji za asili, tutaendelea kuuhamasisha ili mradi tu tuweze

kuutumia kisayansi na tuweze kufikia malengo yetu. Tusingependa kuwa tutumie tu mbolea ya mboji, tutumie tani 20 kwa hekta wakati hata mkulima hawezi kuifikisha kwa haraka. Kwa hiyo tutatumia zote mbili kwa pamoja na tutaendelea kutumia utaratibu huo wa kuhamasisha.

Na. 8

**Vipimo Halali vya Ununuzi wa Mazao ya Wakulima**

**MHE. BRIG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI** aliuliza:-

Kwa kuwa wakulima wa maeneo ya vijijini katika Wilaya ya Lushoto hulazimika kuuza mazao yao ya mashambani kama mahindi, maharage, mboga na kabichi, karoti, viazi, matunda kwa kutumia ujazo wa gunia na hata magunia mawili yaliyounganishwa maarufu kwa jina la Lumbesa:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ununuzi wa mazao ya mashambani kwa kutumia vipimo vya ujazo badala ya vipimo vya uzito ni njia mojawapo ya kumdhulumu na kumkandamiza mkulima?

(b) Je, Serikali inatoa maelekezo gani kwa Watanzania wote hususan Halmashauri za Wilaya na Serikali za Vijiji kuhusu vipimo halali vya ununuzi wa mazao ya wakulima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu! Huyu naye namtambua kuwa ni Naibu Waziri mpya katika hiyo Wizara. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba nitoe maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inazo taarifa za kuwepo mtindo mbaya unaotumiwa na baadhi ya wanunuzi wa mazao ya kilimo yakiwemo hayo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge wa kujaza magunia kupita kiasi ambao wao wanauita Lumbesa au Kosovo. *(Makofi)*

Uchunguzi uliofanywa na Wizara yangu umebaini kuwa ujazaji wa aina hiyo wa Lumbesa au Kosovo hutumiwa kwa madhumuni ya kupunguza gharama za usafirishaji kwenye vyombo vya uchukuzi ambao hutoza gharama kwa kuhesabu magunia badala ya uzito. Aidha, wakati ulipokuwepo utaratibu wa kutoza ushuru wa mazao wakati wa kusafirisha kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, ushuru huo pia ulitozwa kwa gunia kama kipimo badala ya uzito; na japokuwa utaratibu wa kutoza ushuru wa mazao yanaposafirishwa ulikwishafutwa, bado kuna baadhi ya wafanyabiashara wanaendelea na utaratibu wa kujaza magunia kwa mtindo huo mbaya wa aina ya Lumbesa au Kosovo.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ununuzi wa mazao ya mashambani kwa kutumia vipimo vya ujazo usio rasmi badala ya vipimo rasmi ni njia mojawapo ya kumdhulumu na kumkandamiza mkulima. Kwa kutambua athari hizo zinazompata mkulima kutokana na utaratibu huo mbaya unaofanywa na baadhi ya wanunuzi; Serikali kwa kutumia Wakala wa Vipimo pamoja na Halmashauri za Wilaya na Miji imekuwa ikisimamia na kuhimiza matumizi ya vipimo rasmi vinavyokubalika kisheria ambavyo ni kilogramu na lita badala ya vipimo visivyo rasmi vikiwemo makopo, mafungu pamoja na ujazo wa Lumbesa au Kosovo.

Aidha, Serikali imeendelea kupiga vita matumizi batili ya vipimo kwa kutoa elimu kwa umma kwa kutangaza kwenye vyombo vya habari yakiwemo magazeti, redio na televisheni pamoja na mikutano.

(b) Mheshimiwa Spika, maelezo ya kukataza matumizi ya vipimo visivyo rasmi yametolewa kwenye sheria ya vipimo Na. 20 ya mwaka 1982 inayosisitiza matumizi ya mizani katika biashara na Wizara yangu kupitia Wakala wa Vipimo inaendelea kusimamia sheria hiyo.

Aidha, Serikali inafanya ukaguzi kupitia Maafisa Vipimo katika mikoa yote kwa lengo la kusimamia matumizi ya vipimo sahihi katika biashara. Wafanyabiasahara wanapopatikana na kosa kama hilo la kutumia Lumbesa, hupewa adhabu chini ya sheria hiyo ya vipimo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara yangu kupitia Kurugenzi yake ya Maasoko na Wakala wa Vipimo inafanya mipango na *TCCIA* na Vyama vya Ushirika kuandaa vituo vya kuuzia mazao ambavyo vitakuwa na mizani ambnayo itatumika kuuzia mazao ya wakulima na kuwezesha ukaguzi kufanyika kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua zote hizo, Serikali inapenda kurudia kusisitiza tamko lake ambalo limekuwa likitolewa mara kwa mara la kupiga marufuku matumizi ya vipimo visivyo rasmi vikiwemo vya ujazo wa Lumbesa au Kosovo. Ni matumaini ya Serikali kuwa Waheshimiwa Wabunge wataunga mkono hatua hizi za Serikali kwa kuwaelimisha wakulima wetu wasiangukie katika mtego huu mbaya wa baadhi ya wafanyabiashara wasiotumia vipimo rasmi. *(Makofi)*

**MHE. BRIG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Vile vile namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, lakini nadhani kama Mheshimiwa Naibu Waziri kama alivyosema kwamba Serikali imekuwa ikitoa maelekezo na inaelekea kwamba suala hili bado linaendelea kuvunjwa. Sasa, atakubaliana nami kwamba ni wakati muafaka kwa

Serikali kuwa kali zaidi kuhakikisha kwamba mtindo huu wa kuwadhulumu wakulima unakomeshwa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana naye kabisa kwamba vitendo hivyo ambavyo vinafanywa na baadhi ya wafanyabiashara hao ni kuwadhulumu wakulima na ndio maana nimesema kwamba ziko adhabu ambazo zinatolewa kwa mujibu wa sheria hiyo na nimetoa mwito hapa kwamba pamoja na kupiga marufuku huko, lakini ushirikiano mkubwa sana unahitajika na wenzetu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kule tuliko pamoja na sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha tunawaelimisha wananchi wetu wasiangukie katika mtego huo mbaya. Lakini, Serikali inataka kusisitiza tu kwamba mtu yeyote atakayepatikana na kosa hilo la kuwadhulumu wananchi kwa kutumia Lumbesa, hatua kali zitachukuliwa.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa suala la Lumbesa ni tataizo sugu na hasa kwa wakulima wa Kitanzania ambao mazao mengi yanalimwa sehemu nyingi kama vile viazi vinavyopatikana mikoa mbali mbali ya Tanzania; na kwa kuwa amebaini kabisa kwamba ipo sheria Na. 20 ya mwaka 1982 ambayo inaonekana wazi kwamba usimamizi wake umeshindwa kukidhi hili tatizo; je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi wakati juhudi zinaendelea kufanyika, basi itolewe sheria kwenye hiyo Na. 20 kwamba kuanzia sasa nchi nzima gunia lolote kama ni la viazi likiwa na Lumbesa, basi litozwe ushuru mara mbili ili kuwakatisha taamaa wanunuzi na hivyo, kuwalinda wananchi wakati sheria bado inatekelezwa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka tu niseme kwamba hii sheria Na. 20 inayohusu Vipimo na Viwango, haijashindwa, kwa sababu kama nilivyokuwa nimesema kwamba inaendelea kusimamiwa na Maofisa wetu na kwamba mtu yeyote anayepatikana na kosa la aina hiyo, adhabu kali hutolewa na nikasema kwamba sasa hivi tunashauriana na vyombo vingine kuhakikisha kwamba vinawekwa vituo maalum kwa ajili ya kuuzia mazao ambayo itakuwa rahisi kukagua. Lakini niseme tu kwamba habari ya kutoza ushuru, kutoza gunia mara mbili, nimesema utaratibu wa kutoza ushuru ulikwishafutwa. Kwa hiyo sasa hivi mazao yanaposafirishwa kutoka sehemu moja hadi nyingine, utaratibu uliokuwa unatumika zamani sasa hivi hautumiki tena. Kwa hiyo, nataka tu nisisitize tu kwamba hatua hizi tunazozichukua zikifanikiwa, nadhani sheria yetu itaendelea kutumika vizuri zaidi.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa matatizo yanayowapata wakulima wa Lushoto, vile vile yanawapata wakulima wa viazi wa Mkoa wa Mbeya hususan maeneo ya Uporoto pamoja na maeneo ya Rungwe pamoja na Makete vile vile na Mbeya Vijijini. Ili kupunguza tatizo hili, je, Serikali inaonaje kwamba umefika wakati sasa wa kuhamasisha wawekezaji ili waweze

kujenga viwanda vya kuweza kusindika viazi katika maeneo hayo na kumwezesha mkulima kuweza kupata faida kubwa zaidi kuliko hali ya sasa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye kwamba wakulima wa maeneo aliyoyataja ya Mbeya na kwingineko, mazao yao makubwa ni viazi na mengineyo ambayo wanapata athari hizi nilizozieleza hapa. Sasa pendekezo lake la kuhamasisha wawekezaji.

Mimi nakubaliana naye moja kwa moja kwamba ni vizuri kuhamasisha wawekezaji katika kuandaa viwanda vya usindikaji ili mazao hayo kwanza yaongezewe thamani, lakini vile vile suala la kulanguliwa lisiwepo.

Mheshimiwa Spika, lakini na pengine napenda tu niongeze kwamba sasa hivi Serikali inatekeleza ile sheria ya Utaratibu wa Stakabadhi za Mazao Ghalani ambayo nayo kwa kiwango kikubwa kama wakulima wetu wataitikia na kutekeleza ipasavyo, inasaidia sana kuepukana na tatizo hili la ulanguzi ambalo wafanyabiashara binafsi wanayafanya kwa wakulima wetu.

Na. 9

**Mtandao wa Barabara za Afrika Mashariki**

**MHE. LAZARO S. NYALANDU** aliuliza:-

Kwa kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, imelenga kuboresha mahusiano ya wananchi na nchi zote tatu; na kwa kuwa mtandao wa barabara za Afrika Mashariki, utawezesha wananchi kuendesha shughuli za kiuchumi na kijamii kwa ubora zaidi.

(a) Je, ni barabara zipi zipo katika mtandao wa barabara za Afrika Mashariki na zina urefu gani kati ya Kenya, Uganda na Tanzania?

(b) Je, Jumuiya inategemea kuanza kazi ya ujenzi wa barabara hizo lini na kwa muda gani hadi kuzikamilisha?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya sijajibu swali la Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) ningependa kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa upya Jumuiya ya Afrika Mashariki kumekuwa na ushirikiano katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Miradi ya barabara zinazounganisha nchi wanachama ni miongoni mwa maeneo ya ushirikiano tangu mwaka 1998. Lengo kuu la mradi wa barabara ni kuimarisha usafiri na uchukuzi

baina ya nchi zetu tatu na hivyo kukuza biashara. Nchi wanachama kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, hutafuta fedha za ujenzi wa barabara kwa kushirikiana. Utekelezaji wa mradi husika hufanywa na nchi mwanachama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, kama ifuatavyo:-

(a) Mtandao wa Barabara za Jumuiya ya Afrika Mashariki una jumla ya kilometa 11,994 ambapo kati ya hizo kilometa, 6,993 ni za Tanzania, Kenya kilometa 3,439 na Uganda kilometa 1,562. Barabara husika katika mradi huo hizi ni zifuatazo:-

(i) Tanga – Horohoro Lungalunga – Mombasa – Malindi – Garissa;

(ii) Arusha – Moshi – Holili/Taveta - Mwatate – Voi;

(iii) Tunduma – Sumbawanga – Kasulu – Nyakanazi;

(iv) Tunduma – Iringa – Dodoma – Arusha – Namanga – Nairobi – Isiolo – Moyale;

(v) Dar es Salaam – Dodoma – Isaka – Mutukula – Masaka;

(vi) Biharamulo – Mwanza – Musoma – Sirari – Kisumu – Kitale – Lodwar – Lokichoggio;

(vii) Mombasa – Malaba – Katuna.

(b) Kumekuwa na maendeleo ya kuridhisha katika kutekeleza mradi wa barabara katika Jumuiya. Kilometa 600 tayari zimejengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilometa 2,582 zimepata fedha kutoka kwa wahisani. Aidha, kilometa 2,081 ziko kwenye hatua ya usanifu. Benki ya Maendeleo ya Afrika imekubali kufadhili mradi wa barabara katika maeneo ya Arusha – Moshi - Holili/Taveta – Mwatate – Voi pamoja na Mombasa – Lungalunga/Horohoro – Tanga.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii, naomba radhi kwa *mic,* ninaomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa utaratibu huu uliowekwa awali tulisikia kwamba barabara inayotoka Minjingu kwenda Babati- Qateshi -Singida na kuendelea Tabora mpaka Kigoma, ilikuwa ni moja ya barabara ilikuwa ni moja ya barabara zilizokuwa kwenye mtandao wa barabara za Afrika Mashariki. Katika majibu ya Naibu Waziri sijasikia kabisa barabara inayotoka Minjingu, Babati, Singida, iendelee mbele mbele na ningeomba kama Mheshimiwa Naibu Waziri, atawathibitishia wananchi wa Singida kwamba barabara yao ipo au haipo na kama haipo inajengwa kwa mfumo upi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu lengo kubwa la Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni kuhakikisha tunaunganisha Afrika Mashariki yote na hiyo imeelezwa wazi katika Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, katika kifungu cha 90 ni barabara zipi zinakuwa ndani ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, hizi zinabadilika kulingana na mabadiliko kulingana na mahitaji na kulingana na hoja zinavyojengwa.

Mheshimiwa Spika, tumemsikia Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, tutaangalia kama barabara hiyo na iwe sehemu ya barabara za Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini vile vile Wizara husika ndani ya nchi tuna mipango mingine ya barabara nina uhakika na Wizara hiyo imelisikia itaangalia tunaweza tukafanya namna gani. Kwa hiyo, kwa kupitia ndani ya Afrika Mashariki tutafanya yale yanayowezekana lakini vile vile na Wizara yetu ya Miundombinu na yenyewe itafanya yale inayoweza.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, asiwe na wasiwasi lengo letu ni maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwa majibu ya ziada ni kwamba napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba barabara ya Minjingu - Babati na Singida ipo na itafadhiliwa na *African Development Bank. (Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nilikuwa na swali kama ifuatavyo:-

Swali la msingi (b) limeuliza Jumuiya inategemea kuanza kazi ya kujenga barabara hizi lini na kwa muda gani? Wakati akijibu swali amesema Tanzania upande wetu tuna kilometa 6,000 lakini mpaka sasa tumefanya kilometa 600. Nilitaka Naibu Waziri aniambie ni mpango upo madhubuti na kwa muda gani kwamba hizi kilometa hizi zilizobaki kati ya 6000 kutoa 600 zitakuwa zimetimilika lini?

**SPIKA:** Waziri mpya wa Miundombinu na ndiye aliyekuwa Waziri wa Afrika Mashariki na Ushirikiano wa Kimataifa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika**,** kwanza niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa makofi hayo. Pili, napenda nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Peter Serukamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli nchi yetu katika mtandao wa barabara za Afrika Mashariki, Tanzania ndiyo zenye kilometa nyingi ambazo zimetajwa 6,000 na ushee. Mpaka sasa ni kilometa 600 ambazo zimeweza kujengwa. Kama Serikali ilivyosema wakati wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii nyingi ya barabara hizi ikiwemo hii ya Arusha, Minjingu, Babati, Singida ndizo ambazo tumekuwa tunazitafutia fedha toka kwa wafadhili. Lakini pia katika mtandao huo zipo barabara nyingine ukiangalia *Central Corridor* kuna kazi ambayo inaendelea ya barabara kutoka Dodoma, Singida - Manyoni na Manyoni - Singida yote hii ni azma ile ile kama ya kutoka Shinyanga mpaka kwenye Mwanza *border* maana tunataka ukanda huu wa *Central Corridor* kama alivyoeleza

Mheshimiwa Naibu Waziri, katika jibu lake tuikamilishe katika sehemu ya mtandao wa barabara zetu ambazo ziko katika mtandao wa Afrika Mashariki. Kwa maana hiyo, kwa kadri ambavyo tutaweza kupata fedha na tunategemea fedha nyingi zitoke kwa wafadhili ambao tunashirikiana nao katika maendeleo ya nchi yetu.

Kwa hiyo, sana kumjibu Mheshimiwa Peter Serukamba, kwamba ni lini tutaweza kukamilisha kilometa 5400 ambazo zimebaki. Lakini tunaamini kwa ahadi ambazo tumezitoa humu Bungeni na jitihada za Serikali ambazo zinaendelea katika kuzitafutia fedha barabara hizi pindi tunapopata uhakika tutaifanya kazi hii kwa sababu bila mtandao huu kuukamilisha miundombinu kama lilivyoulizwa swali hapa asubuhi bila kuwa na miundombinu ya uhakika kuunganisha nchi zetu tatu hatutakuwa tunafanyakazi kubwa ya kuunganisha nchi yetu. Lakini kubwa zaidi katika kuhakikisha Tanzania tunaweza kuibua uchumi wa haraka nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante kwa kuzingatia muda tunaendelea Wizara hiyo hiyo, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, hayupo kwa niaba yake Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Kwa niaba yake Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, naomba swali lake namba 10 sasa lijibiwe. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona kidogo Spika ameghafilika, isingekuwa vema kwa utaratibu wetu kwamba Mheshimiwa Dr. Slaa awe badala ya Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni aliulize hilo swali. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Kwa niaba ya Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, naomba swali lake namba 10 sasa lijibiwe. *(Makofi)*

Na. 10

**Majadiliano Juu ya Mahusiano ya Kiuchumi na *EU/EPA***

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni Mjumbe wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na kwa kuwa nchi wanachama wa Jumuiya hiyo ziko kwenye majadiliano ya mahusiano ya kiuchumi na Umoja wa Ulaya *(EU)* yaitwayo *EPA* katika makundi mbalimba kama vile Tanzania na *SADC-EPA*, na Kenya na Uganda – *ESA;* na kwa kuwa hizi *EPAs* lazima zitumike mahali penye Muungano wa Forodha, kwa mfumo huo hawaruhusu nchi yoyote kuwa mwanachama kama nchi hiyo si mjumbe wa Muungano wa Forodha moja na siyo zaidi:-

(a) Je, Serikali haioni kwa kuendelea na majadiliano chini ya *SADC-EPA* kutaleta katika kukubalika kwa yale ambayo yamekwishafanyika chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kama vile mambo ya Muungano wa Forodha?

(b) Je, hali hiyo haitapunguza hadhi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kama Tanzania itaingia Mkataba wa *SADC-EPA* na Kenya na Uganda zikaingia Mkataba wa *ESA-EPA* na kufanya seti mbili tofauti za *Tariff Elimination Commitment?*

(c) Je, kwa nini Tanzania tusihamie kundi la *COMESA* ili kuungana na wenzetu wa Kenya na Uganda kwa pamoja chini ya mpango wa nchi za *ESA?*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, ningependa kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mfumo wa baadaye wa mahusiano kati ya nchi za Asia, *Pacific* na *Caribbean (ACP)* na Muungano wa Ulaya, ni suala la majadiliano. Muungano wa Ulaya ulipendekeza kwamba itakuwa bora zaidi endapo kanda za majadiliano zitakuwa zimefikia hatua ya soko la pamoja na katika mtangamano. Kinadharia nchi haiwezi kuwa mwanachama wa Umoja wa Forodha zaidi ya mmoja. Lakini kivitendo inawezekana ili mradi Umoja wa Forodha husika ziwe na sera sawa za biashara ya nje au kuwepo na mpango wa muda mrefu wa kuoanisha sera za biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhana ya ushirikiano katika Bara la Afrika, ni pana zaidi kwa maana ya kwamba ushirikano wa kikanda ni nyenzo tu ya kujenga umoja wa Afrika. Kwa mantiki hiyo, mipaka ya kikanda si ya kudumu. Kwa upeo wa muda mrefu, *SADC, COMESA* na *EAC* hazina budi kuhuisha sera zao ili kujenga ushirikiano unaojumuisha nchi nyingi zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, kama ifuatavyo:-

(a) Kuendelea na majadiliano chini ya *SADC-EPA* hakutaleta matatizo. Kwanza, nchi za Afrika Mashariki zilikubaliana kuwa na msimamo mmoja katika masuala yote yatakayojadiliwa katika *EPA*. Kwa hiyo, kuna mashauriano ya karibu sana kila wakati.

Mheshimiwia Spika, pili, Kanda za *SADC-EPA* na *ESA-EPA* hushauriana kwa lengo la kutotofautiana kimahusiano miongoni mwao na Muungano wa Ulaya *(EU).*

(b) Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, inazitaka nchi wanachama kutokuingia mikataba inayopingana na malengo na taratibu za Umoja wa Forodha. Kwa hiyo, tahadhari zimechukuliwa na kuepuka uwezekano wa mingongano kutokea. Mathalani, Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki lili agiza Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuainisha maeneo ambayo *EAC* itahitaji kujadiliana na kanda za *SADC* na *COMESA* ili kuondoa tofauti za kisera.

(c) Kuhamia *COMESA* si jawabu la changamoto zitokanazo na ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya za Kikanda za Maendeleo. Hatua hiyo itadhoofisha juhudi za kuunda jumuiya mpya ya Afrika Mashariki na vile vile mtangamano katika Bara la Afrika. Kwa hiyo, hatua muafaka ni ile inayolenga katika kuihisha sera na mipango ya mtangamano ya kanda tatu za *SADC*, *EAC* na *COMESA*.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yenye ufafanuzi wa kina wa Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa ni dhahiri kwamba Tanzania tulikuwa wanachama wa *COMESA* na baadaye tukajitoa kwa faida ambazo tulidhani kwamba kwa wakati ule zilikuwa ni sahihi. Lakini vile vile ni kwamba sasa hivi ni wanachama wa *SADC*, Kenya na Uganda ni wanachama wa *COMESA.* Wakati huo tunaendelea na suala la *Economic Partnership Agreement* kwenye mambo ya *EPA* sasa sielewi sasa katika mchakato mzima wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, unavyoendelea sasa hivi na hizi *economic differences* Tanzania tutakaa katika *position* ipi ikiwa wenzetu wa Kenya na Uganda wana lugha ya *COMESA* na sisi tuna lugha *SADC*. Je, Serikali haioni kwamba ni muda muafaka wa kufanya mkakati wa haraka iwezekanavyo kutathmini *position* ya Tanzania na hasa ukizingatia kwamba sasa tunaingia kwenye shirikisho la Jumuiya ya Afrika Mashariki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mpya wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa makofi ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, katika mahusiano ya Kimataifa mahusiano ya Kanda hujengwa kutokana na historia na maslahi ya nchi zinazohusika. Tuliingia *SADC* kama waanzilishi kwa sababu ya historia yetu na maslahi ya nchi yetu na tuko *SADC* kwa sasa na naamini tutaendelea kuwepo *SADC* hadi hapo itakapoonekana kwamba maslahi ya nchi hayalindwi vizuri.

Lakini la pili, ni kwamba hata katika hizi nchi nyingine hakuna nchi yoyote ile ambayo iko katika kanda moja tu. Nchi zote ziko katika kanda mbalimbali kama nilivyosema awali kutokana na historia na maslahi ya nchi.

Kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri, amejibu vizuri sana asubuhi hii hapa ni kwamba pamekuwa na uelewa wa pamoja kwamba pamoja na kwamba Uganda na Kenya wako katika mkondo mwingine na sisi tuko katika mkondo mwingine lakini yapo maelewano kwamba lazima pawe na ushirikiano kuhakikisha kwamba maslahi ya pamoja ya nchi hizi zote yanalindwa na yanatiliwa maanani.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo linapaswa kufahamika ni kwamba ujenzi wa kanda kama ambavyo sera yetu inavyoeleza ni kama hatua, kama ni ngazi ambapo hapo

baadaye sote kama nchi za Kiafrika tunatakiwa tuunde Jumuiya ya Uchumi wa Afrika. Kwa hiyo, imekuwa kama ni njia za mpito. Lakini hakuna hasara ya sisi kuwa katika Kanda ya *SADC* na wenzetu kuwa katika kanda nyingine.

Mheshimiwa Spika, mwisho juu *COMESA* kama ambavyo Mheshimiwa muuliza swali Dr. Chegeni, amesema Tanzania ilikuwa mwanachama wa *COMESA*, ilijitoa kutokana na ushauri na muono wa maslahi yetu kwa wakati huo na maslahi ni jambo ambalo ni kama mchakato au jambo ni la kuendelea ukifika wakati tukaona kwamba kuna haja ya kuleta usawazisho wa aina fulani ama kwa kutazama tena *COMESA* namna gani ilivyo au kwa njia nyingine yoyote mimi naamini kabisa nchi yetu inazingatia sana maoni ya wadau wake katika sera yake ya mambo ya nje na katika ushirikiano wake wa kanda na tutafanya hivyo. *(Makofi)*

Na. 11

**Tatizo la Maji Jimbo la Ilala**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina mikakati mizuri ya kushughulikia tatizo la maji nchini; na kwa kuwa mipango hiyo itachukua muda mrefu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku maalum katika Jimbo la Ilala, kujenga visima virefu ili kupunguza tatizo hilo linalosababisha kero kubwa hasa ugonjwa wa kipindupindu, ukizingatia kuwa uwezo wa Halmashauri ni mdogo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Zungu, Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Ilala pamoja na maeneo mengine ya Jiji la Dar es Salaam hupata maji safi ya bomba kupitia kwenye mfumo wa maji safi unaotegemea maji ya Mto Ruvu na visima vya kina kirefu na kifupi. Mfumo huo unakabiliwa na matatizo yafuatayo:-

(i) Uwezo mdogo wa mitambo ya kuzalisha maji usiolingana na mahitaji. Kiasi cha maji kinachozalishwa kwa vyanzo vya Ruvu Juu, Ruvu Chini, Mtoni na visima ni mita za ujazo 270,000 kwa siku ambazo ni asilimia 60 tu ya mahitaji ambayo yanafikia mita za ujazo 450,000 kwa siku.

(ii) Upotevu mkubwa wa maji ambao ni asilimia 55 ya maji yote kutoka kwenye vyanzo. Upotevu huo unatokana na uvujaji wa mabomba na wizi wa maji.

(iii) Kuharibika mara kwa mara kwa mitambo ya kusukuma maji unaotokana na uchakavu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa katika baadhi ya maeneo ya Jimbo la Ilala, kama ilivyo katika maeneo mengine ya Jiji la Dar es Salaam, kuna matatizo ya ukosefu wa maji. Ili kukabiliana na matatizo haya ya upungufu wa maji, Serikali kupitia *DAWASA* inatekeleza mpango kapambe wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya kusambaza maji safi na uondoaji majitaka. Ukarabati na upanuzi huo utagharimu shilingi bilioni 164. Mradi huo ulianza mwaka 2003 na utakamilika mwishoni mwa mwaka 2008.

Katika jimbo la Ilala maeneo ya Mchikichini, Buguruni na Ilala yenyewe yatahusika. Aidha, mpango wa maji unaozihusisha Jumuiya za wananchi *(Community Water Supply and Sanitation Program)* ambao unasimamiwa na asasi isiyo ya Kiserikali ya *Plan International*, utekelezaji katika maeneo ya Markaz, Biblia Relini, Majumbasita Bondeni, Mzinga A, Mzinga B, Ulongoni, Gulukwa, Kwalala, Korongoni na Katezenge katika kila eneo kutachimbwa kisima, kujengwa tanki na kufungwa bomba la kusambaza maji majumbani. Mradi huu utagharimu shilingi milioni 650 na utakamilika mwishoni mwa mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, mbali na miradi hii kuna uchunguzi unaofanywa na kampuni ya *Nor Consult* juu ya vyanzo vya maji kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam likiwemo Jimbo la Ilala. Katika uchunguzi huo visima vitatu vya kina kirefu vitachimbwa katika maeneo ya Mpiji, Kisinga na Kimbiji. Aidha, uchunguzi kwa ajili ya ujenzi wa Bwana la kuhifadhi maji ya Mto Ruvu katika eneo la Kidunda Mkoani Morogoro, utakaofanyika mwaka huu wa fedha wa 2006/2007. Baada ya uchunguzi kukamilika ujenzi wa bwawa hilo unatarajiwa kuanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Serikali kuwa baada ya miradi yote hii kukamilika, maeneo mengi ya Jimbo la Ilala, yatapata maji safi na salama ili kuondokana na kero za ukosefu wa maji na ugonjwa hasa wa kipindupindu.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kutia imani. Lakini mwaka 2008 bado ni mbali sana. Tunaomba kwa hali ilivyokuwa sasa hivi ombi letu kwa Serikali kutusaidia baadhi ya maeneo kupata maji safi katika Jimbo la Ilala litiliwe mkazo na maeneo mengi aliyotaja Mheshimiwa Waziri si maeneo ya Ilala ni maeneo nje ya Jimbo la Ilala.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Jiji la Dar es Salaam lina upungufu wa maji na jitihada mbalimbali zinafanywa mimi nikiwa ni mmojawapo ambaye nimezunguka sana kuangalia sehemu mbalimbali zikiwemo sehemu nilizozitaja na pia na kwa hivi sasa tumezungukia maeneo ambayo tunayaita ni *peri urbun* ambayo maeneo mengi hayo bado yana visima vichache vya maji. Lakini mimi napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge ya kwamba zaidi ya juhudi hizo zilizo na pia Mheshimiwa Mbunge, aangalie uwezekano mkubwa kwa kutumia *Plan International* ambao sasa hivi wanatoa maji katika jumuiya mbalimbali za Jimbo la Ilala.

Mheshimiwa Spika, tumewagawa hawa katika mafungu, kuna ambao wenyewe wanafanya katika Wilaya ya Kinondoni lakini katika Wilaya ya Ilala hawa *Plan*

*International* wanafanyakazi nzuri. Mimi mwenyewe nimeshuhudia katika maeneo yakiwemo ya Biblia Relini na Markaz nimetembelea visima ambavyo ni vizuri na vinakidhi mahitaji katika sehemu kubwa. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awatumie hawa kwa sababu ni njia mojawapo ya karibu na njia nyingine itabidi tushughulikie na tusubiri hiyo mipango ambayo nimeshaiorodhesha hapa awali. *(Makofi)*

Na. 12

**Ahadi ya Serikali kwa Ajili ya Huduma ya Maji Arumeru Magharibi**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER (k.n.y. MHE. ELISA D. MOLLEL)** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Arumeru Magharibi wana shida kubwa ya maji safi na salama kwa matumizi ya binadamu na kwa kuwa wananchi wa Kata sita waliokuwa wanatumia maji ya Mto Nduruma waliridhia maji hayo yatumike kwa wakazi wa Jiji la Arusha kwa ahadi ya Serikali kwamba watapewa shilingi milioni mia moja kuwawezesha kuchimba visima na kujenga miundombinu ya kusambaza maji katika Kata za Bangata, Sokon, Moshonu, Mlangirini, Nduruma na Bwawani:-

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ili kuwapunguzia wananchi wa Kata hizo sita adha ya ukosefu wa maji safi na salama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elisa Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Serikali iliahidi kutoa fedha kwa ajili ya kuwapunguzia wananchi wa Arumeru Magharibi kero ya maji. Katika juhudi za kutimiza ahadi hiyo Wizara imeitumia Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru shilingi milioni 20. Shughuli zilizofanyika kwa kutumia fedha hizo ni ujenzi wa tanki la maji lenye uwezo wa kuhifadhi galoni 10,000 katika Kijiji cha Oldadai, Kata ya Sokon II, ununuzi wa mabomba kwa ajili ya mradi wa maji wa Nduruma, ujenzi wa uzio wa chanzo cha maji cha mradi wa maji Baraa – Moshonu na ujenzi wa chanzo cha maji cha Meefu, Kata ya Nkwandua.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru, imepanga kutekeleza miradi ya maji katika Jimbo la Arumeru Magharibi mwaka huu wa fedha 2006/2007 chini ya programu ya Kitaifa ya maji na usafi wa mazingira vijijini kama ifuatavyo:-

(i) Itakarabati miradi katika vijiji vya Moshono, Mulangirini, Nduruma na Olgilai ambayo itakayogharimu jumla ya shilingi milioni 58.

(ii) Itaanza usanifu wa miradi katika vijiji vya bwawani, Matova, Losikito, Muriet na Ngorbobi kwenye Jimbo la Arumeru Magharibi. Usanifu utafuatiwa na ujenzi wa miradi hiyo niliyoorodhesha.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshauri Mheshimiwa Mbunge kama kiongozi katika Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru kuyapa kipaumbele maeneo yenye adha kubwa ya ukosefu wa maji wakati wa kuandaa bajeti ya mwaka ya Halmashauri ili kuwapunguza adha ya ukosefu wa maji safi na salama wananchi wa jimbo lake.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, jimbo la Arumeru Mashariki au Wilaya nzima ya Arumeru wana matatizo maji salama kwa sababu maji ya mtiririko kutoka Mlima Meru karibu asilimia kubwa siyo salama na kwa kuwa *water table* katika Wilaya ya Arumeru iko juu.

(a) Je, Serikali hawako tayari kuchimba visima virefu katika Wilaya hiyo na hayo maji ambayo siyo salama yatumike kwa umwagiliaji?

(b) Kwa kuwa vijiji vingi viko katika mradi wa *World Bank* na *World Bank* mradi huo unaweza ukasaidia vijiji vingi. Je, huo mradi wa *World Bank* utakuja lini ili kufaidisha vijiji hivyo pamoja na Jimbo la Longido analosubiri? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika miradi hii ya sasa tunajitahidi sana kuchimba visima virefu ambavyo ni salama lakini pia ni wajibu wa kila Wilaya na kila kijiji wakati tunapowatuma wataalam wetu kwenda kuangalia aina gani ya mradi inahitajika ili wenyewe waeleze wachague aina ya mradi ambapo wanaweza wakachagua visima virefu au wakachagua bwawa au wakachagua kutengenezewa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, hivyo ni kwamba naomba Mheshimiwa Mbunge atusaidie Wizara yetu kuhamasisha wananchi wakati wanapochagua aina ya mradi. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mradi wa *World Bank* katika Arumeru nzima kwa upande wa Arumeru Mashariki miradi hii ambayo ndiyo sasa hivi itatekelezwa ikiwemo Ambureni, Mwaivara, Mbuguni, Vilasika, Kikulelwa na King'ori na kwa upande wa Arumeru Magharibi, itakayoshughulikiwa kwa sasa hivi ni Bwawani, Matova, Losikito, Muryeti na Ngoribobi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Katika eneo hili la maswali nimekumbushwa na Mheshimiwa Halima Mdee, kwamba katika Mkutano wa Nne wakati yeye hayupo swali lake liliulizwa na Mheshimiwa Gosbert Blandes wa Karagwe. Pale pia nilighafilika, kwa utamaduni wa Mabunge yetu katika *Commonwealth* si vizuri upande mmoja ukajaribu kuuliza swali la upande mwingine. Huu ni utamaduni tu, haimo kwenye Kanuni, lakini ni utamaduni kwa sababu mara nyingi malengo ya pande hizi mbili hayalingani. Kwa hiyo, ni vizuri tukakaa hivyo na kwa sababu tuko kwa

pande zote Wabunge wa kutosha basi huo ndio utakuwa mwongozo kuanzia sasa. Spika, anawaahidi hataghafilika tena. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima kubwa sana naomba pale kwenye *Speaker's Gallery* nitambue uwepo wa Mbunge kutoka nchi rafiki ya Sweden, Mheshimiwa Henrick Westman. *(Makofi)*

Amekuja kwa ziara ya siku moja kuona jinsi Bunge letu linavyofanya kazi na tunamkaribisha sana pamoja na mwenyeji wake Bwana Arinesi Venson ambaye ni Mtaalam wa Kampuni inaitwa *Profesional Management.* *(Makofi)*

*Honourable Westman, we welcome you to Dodoma. We feel very honour to have a guest from Sweden, a country with which we enjoy the most codual reletions. Thank you and have a good stay. (Applause)*

Upande wa kulia wa Spika katika *Gallery* wapo viongozi waandamizi wa chama cha CHADEMA kutoka Makao Makuu Dar es Salaam, naomba wasimame ili waweze kutambuliwa. Karibuni sana Waheshimiwa. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Wabunge wa CCM Zanzibar ameniomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM kutoka Zanzibar kutakuwa na kikao leo saa 7 mchana katika chumba namba 428, Wabunge wa CCM kutoka Zanzibar saa 7 mchana chumba namba 428.

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ameniomba nitangaze kwamba Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wakutane mara baada ya kipindi hiki cha maswali katika ukumbi namba 231 kuzingatia Miswada mitatu ambayo iko mbele ya Kamati yao. Ukumbi namba 231 mara baada ya kipindi hiki cha maswali, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa James Musalika, Mwenyekiti wa *Tanzania Chapter* ya *Amani Forum* anawaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji ya *Amani Forum* wakutane mara baada ya kipindi hiki cha Maswali na Majibu Ukumbi wameutaja ni 231 ambao unagongana na Ukumbi mwingine. Kwa hiyo, Katibu utasimamia utaratibu ili hawa waingie katika Ukumbi mwingine.

Wabunge wa Mkoa wa Iringa ile safari ya kwenda Iringa kwa ajili ya mazishi ni leo saa 7.20 mchana, Ofisi ya Bunge imeweka *basi* maalum kwa hiyo mtaweza kuondoka saa 7.20 mchana nje ya Ukumbi wa Bunge. Tangazo hili nimeletewa na Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, lakini pia na Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mbunge wa Kalenga. Mheshimiwa Stephen Galinoma naye alileta tangazo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, tutatafuta muda tuweze kupata maelezo ya kutumia hizi kadi. Kwa maana ya mazungumzo lakini muhimu zaidi pia ni wakati wa kupiga kura itakapoamuliwa tupige kura kwa kutumia kadi yaani *electronic votting* basi na maelezo yake. Kwa hiyo, tutatafuta muda ili tuweze kuzitumia hizo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba kutambua uwepo wa mwenzetu Mbunge wa Kilwa Kaskazini, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, ambaye yupo karibu na Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, pale.  Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, ningeomba usimame tafadhali.  *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mwenzetu huyu kwa bahati mbaya maisha yake yote yamekuwa hana ulemavu.  Lakini kwa kudra za Mwenyezi Mungu imetokea hivyo. Mtakumbuka hakuwepo kikao cha Mkutano wa Pili, wala wa Tatu wala wa Nne.  Lakini kwa taarifa kwa Spika, alikuwa anaendelea kupata matibabu na bado kuna jitihada za Serikali aendelee kupata matibabu.  Nadhani naweza kutamka hapa kwamba Mheshimiwa Rais ameagiza Serikali ifanye utaratibu Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, aweze kupelekwa  nchini Cuba ambako ndiyo kuna wataalam wazuri sana wa eneo hili la magonjwa ya macho.  Namtakia kwa niaba yenu, namtakia ujasiri na kuwatuliza familia yake na ndugu na jamaa, marafiki hali hizi hutokea, lakini tunaamini kwa sababu jitihada bado zipo za kumsaidizi, Mwenyezi Mungu atazibariki ili ziweze kuzaa matunda na mwenzetu arudi kuona.

Kwa sasa hivi nimeamua kwamba kwenye kiti kilicho wazi mbele tu ya *Serjeant-At-Arms* hicho ndiyo kitamfaa kwa urahisi zaidi kwenda katika huduma mbalimbali. Kwa hiyo, nimemwagiza Katibu leo asubuhi atafute msaidizi wa kumsaidia.  Tukishakuwa na Msaidizi pengine kuanzia kesho basi Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, atakaa pale mbele tu ya *Serjeant-At-Arms* ili aweze kuhudumiwa kwa urahisi zaidi.  *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo naona shughuli zilizopangwa kwa leo zimekwisha, kwa sababu Kamati bado zinaendelea kuzingatia Miswada iliyo mbele ya Kamati.  Kwa hiyo, naomba kutamka kamba sasa naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 04.37 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,*
*Tarehe 1 Novemba, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*